# TARGETER WINGS

## JUNIOR SCHOOL ASSESSMENT

# GREDI YA NANE - 2024

Wings 005

## KISWAHILI

**Muda: Saa 1 dakika 20**

**Jina** ______________________________

**Shule** ______________________________

**Nambari ya Usajili:** ____________________ **Tarehe** ____________________

**Maagizo**

*(a) Andika jina lako, la shule, nambari ya usajili na tarehe kwenye vihasho uliopewa.*

*(b) Jibu maswali yote kwenye karatasi hili.*

| MTAHINI PEKEE | | | |
|---|---|---|---|
| **Swali** | **Upeo wa alama** | **Alama ya mwanafunzi** | **Kiwango cha utendaji** |
| 1-29 | Alama 50 | | |
| **Jumla** | **50** | | |

**I. UFAHAMU WA KUSOMA**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi 4:***

Harusi ya nyani ilitia fora sana. Baada ya matayarisho ya takribani miezi saba, hatimaye siku iliyosubiriwa kwa hamu na hamumu iliwadia. Kwa kweli hauchi hauchi unakucha.

Tarumbeta, ngoma, parapanda na aina nyingine ya ala za muziki zilisikika kwa umbali. Wanyama wote walijua mashemeji wamefika. Tayari nyani alikuwa amevaa gauni jeupe pepepe, lililomchukua vyema. Nyweleni utaji ulimetameta metu metu huku shungi lake la nywele likiangukia mabegani. Sauti za akina mbweha na swara zilipokaribia, wanyama wote wakajua siku ya siku imefika.

Nyani alitazama mkoba uliopakiwa nguo zake na kuanza kulengwalengwa na machozi. Mama yake akaanza kutiririkwa na machozi kwa uchungu. Katika boma la mzee nyani, wageni walipokelewa kwa shangwe na nderemo. Bintiye nyani angefunga pingu za maisha. Mavumbi yalitifuliwa, sauti zilipazwa na ala zilichezwa. Kila upande ulijibidiisha kuonyesha umahiri wake. Baada ya mapatano, vigelegele vilihanikiza kote hasa kutoka upande wa wageni.

Machozi ya bintiye nyani yasingezuilika. Dada zake nao wakajiunga naye. Hata hivyo, sungura na simba waliwahimiza wafute machozi maadamu mchumba alikuwa akiishiwa subira kanisani. Wapambe waliongoza njia. Baba wa mchumba wake wakakumbatiana ishara ya kuridhia mwafaka wao.

Bi. harusi alipanda farasi maridadi kuelekea kanisani, wanyama waliachwa midomo wazi wasiamini macho yao. Mavumbi yalipotulia wanyama wote walitulia tuli kumngoja padre ndovu kuanza shughuli.

1. Unadhani kuwa ni kwa nini harusi ya nyani ilitia fora?

______________________________

2. Kwa nini Bi. harusi alilengwalengwa na machozi alipoutazama mkoba uliopakiwa nguo zake?

______________________________

3. Simba na sungura hawakutaka Bi. harusi na dada zake waendelee kulia kwa kuwa

______________________________

4. Unafikiri mapatano yasingeafikiwa ni jambo gani ambalo lingetokea?

______________________________

**II.** ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 5 hadi 8.***

Mungu amejalia binadamu vipawa mbalimbali. Kuna walio na mikono mizuri ya usanii, kuna walio bora katika riadha. Kunao pia wenye vichwa vyepesi vya kushika masomo, kuna waghani wenye sauti za ninga wanaoweza kumtoa nyoka pangoni kwa nyimbo zao tamutamu. Ni imani yetu sote kuwa hakuna yeyote asiyejaliwa angalau kipawa kimoja.

Walemavu nao pia wamejaliwa vipawa mbalimbali. Kunao wasio na mikono wala miguu lakini ni wachoraji hodari kwa michoro yao ya kuajabia. Usanii wao ni wa kipekee. Tunao vipofu lakini huimba kama malaika. Wanao ushupavu kucheza pia ala za muziki. Viziwi wasiosikia wala kuongea nao wakianza kuwasiliana kwa lugha yao ya ishara utabaki mdomo wazi usielewe wanachosema ng'o! utabaki pale kama mjinga wakicheka kumbe ni wewe wanatania.

Walemavu wana nafasi yao katika shughuli zote za ujenzi wa taifa. Wanapaswa kujiona kama raia yeyote maadamu wamepewa vipaji wanavyoweza kutumia kuyakimu maisha yao. Wasio na ulemavu nao pia wajue ni vilema wa aina nyingine. Ikiwa huwezi kuchora, kushona au kuimba, hayo ndiyo mapungufu yako; ulemavu wako.

Walemavu kwa wasiokuwa walemavu watambue kuwa mtu hula jasho lake. Tusiwe wavivu na kutarajia tufanyiwe mambo na wengine. Tutambue na kupalilia vipawa vyetu mapema. Tuvipige msasa vitusaidie sisi wenyewe, jamii na taifa letu.

5. Kulingana na aya ya kwanza, kila mwanadamu amejaliwa nini?

_______________________________________________

6. Je kulingana na kifungu hiki mlemavu hasa ni nani? Mtu ____________
   A. asiye na uwezo wa kutumia sehemu fulani ya mwili
   B. asiyeweza kutekeleza jambo fulani
   C. yeyote asiyeweza kutekeleza jambo fulani
   D. yeyote aliye na kipaji ila hakitumii.

7. Tunapaswa kuviboresha vipawa vyetu, unadhani ni kwa nini tufanye hivyo kulingana na aya ya mwisho?

_______________________________________________

8. Chagua mlemavu aliyeambatanishwa ipasavyo na ulemavu wake
   A. Kipofu - haongei.
   B. Kiziwi - hasikii.
   C. Kiwete - haoni.
   D. Bubu - hatembei.

**III.** **UFUPISHO**

***Soma kifungu hiki kisha ujibu swali la 9 hadi 12.***

Mwanadamu ana haki zake ambazo zimeelezwa vizuri katika katiba ya nchi yetu. Mfano, kila mtu ana haki ya kuishi, kutangamana, kuabudu, kujieleza na hata kuhakikishiwa usalama na nchi. Tunapoangazia haki zetu hasa ya kujieleza, tunapaswa kuhakikisha kuwa hatunyimi mtu mwingine haki zake. Hivyo basi si rahisi kuzungumzia haki zako bila kuzingatia jukumu ambalo unapaswa kufanya.

Watoto huwa na haki zao. Katika kutendewa haki, mtoto ana jukumu la kutekeleza. Ni jukumu la mtoto kuwaheshimu wakubwa wake wakiwemo walezi na wazazi wake. ***Vilevile, mtoto ahakikishe kuwa anawajibika katika kuleta upendo na maelewano katika familia na kuchangia pia katika ujenzi wa taifa***.

Wazazi wana wajibu wa kuwatunza wana wao kwa kuwapatia usalama, lishe bora na mazingira yanayofaa ili kumwezesha kukua vyema. Ni kinyume cha sheria kwa mzazi kumtelekeza mtoto. Serikali imara huhakikisha kuwa watoto wote wametunzwa.

9. Andika kichwa cha kifungu hiki. _______________________________

10. Maneno, ***'vilevile, mtoto ahakikishe kuwa anawajibika katika kuleta upendo na maelewano katika familia na kuchangia pia katika ujenzi wa taifa'*** yanaeleza majukumu ya mtoto. Andika majukumu haya kwa maneno yasiyozidi 12.

_______________________________________________

11. Andika habari kuu inayojitokeza katika aya ya mwisho kwa sentensi moja.

_______________________________________________

12. Wakati wa mgomo wa madaktari, askari alimpiga risasi mmoja wa madaktari akafa walipokuwa wakiandamana. Taja haki mbili zilizokiukwa katika maandamano hayo.

_______________________________________________

## IV. TAMTHILIA

13. ***Sehemu hii ina dondoo lililotolewa kutoka kwenye moja kati ya tamthilia zilizoidhinishwa kwa wanafunzi wa Gredi ya 8. Jibu maswali yote ya dondoo hili.***

| | | |
|---|---|---|
| **Mishi** | : | Nyumba nayo imekufanya nini? |
| **Mabula** | : | Hizi nyumba za kubabaisha humfanya mtu kukunguwaa kwa kukosa level. Nyumba yenyewe wasiwasi kama walioitengeneza... |
| **Mishi** | : | Bila kibanda hiki leo ungeficha uso wako wapi? Ungejisitiri wapi? ***(Kimya kifupi)***. Umesahau mara? Mbona umekuwa mwepesi wa kusahau? |
| **Mabula** | : | Sikiliza Mishi nikuambie. "It is just a matter of time" na mimi nitakuwa "where I belong". |
| **Mishi** | : | Unapopastahili ni wapi ikiwa hata mwiko wa kupikia karibu tutaomba? Mabula, amka bwana! Toka katika ndoto. |
| **Mabula** | : | Mimi ninakuambia ukweli wewe unaona bure. Unayaona yote kuwa mzaha. |
| **Mishi** | : | Ukweli gani? Unayashikilia ya jana kana kwamba ndiyo ya leo. Hata ukuti hukubali kuyumbishwa na upepo bwana. |
| **Mabula** | : | ***(Anashtuka. Anamkazia macho Mishi)***. Huo ukuti una nini? Kila wakati ukuti ukuti! Hata na hao watoto wajualo kuimba ni ukuti. Hakuna nyimbo nyingine za kuimbwa? |

a) Taja mandhari ambayo yanayojitokeza katika dondoo hili. (alama 1)

_______________________________________________

b) Eleza sifa tatu za Mabula kulingana na dondoo hili. (alama 3)

i) _______________________________________________

ii) _______________________________________________

iii) _______________________________________________

c) Eleza masuala mawili yanayojitokeza katika dondoo hili

_______________________________________________

d) Mwandishi wa dondoo hili ametumia mbinu za lugha. Zitaje tatu (alama 3)

i) _______________________________________________

ii) _______________________________________________

iii) _______________________________________________

## V. SARUFI

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 14 hadi 18. Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Siku za hivi karibuni maadili___14___na vijana wengi.___15___ kutoka kwa vyombo vya habari na mtandao___16___. Mila na utamaduni___17___ni tofauti na wazungu. Sote___18___kuwasaidia wengi wa vijana wetu ambao wamejiingiza katika uhalifu wa mtandaoni.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 14. | A. zimepuuzwa | B. yamepuuzwa | C. limepuuzwa | D. imepuuzwa |
| 15. | A. Wanaiga | B. Wakiiga | C. Wanaoiga | D. Wanayoiga |
| 16. | A. yanawapotosha | B. unawapotosha | C. yanapotea | D. vinapotea |
| 17. | A. zetu | B. wetu | C. chetu | D. yetu |
| 18. | A. tuchange bia | B. tupige mbiu | C. tutie fora | D. tufanye itifaki |

19. Tumia kivumishi kwenye mabano kukamilisha sentensi.
Mjomba ______________ alimnunulia tarakilishi mpya. (-ake)

20. Chagua nomino iliyo katika ngeli ya U - U kutoka kwenye kadi hii

| |
|---|
| **Upishi** |
| **Usalama** |
| **Ulezi** |
| **Ugonjwa** |

21. Kinyume cha neno panda ni shuka. Je, kinyume cha neno tabasamu ni ________________

22. Sentensi, 'Nyanya ametembelewa na wajukuu wake' ipo katika kauli gani?

________________________________________

23. Bainisha matumizi ya alama ya mshazari katika sentensi ifuatayo.
Mgeni anaweza kunywa chai/maji.

________________________________________

24. Tunga sentensi katika wakati uliopita hali timilifu ukitumia kitenzi imba.

________________________________________

25. <u>**Yuyu huyu**</u> ndiye aliyetuzwa na mgeni wa heshima. Maneno yaliyopigiwa mstari huitwaje?

________________________________________

26. Andika usemi taarifa ufaao wa: 'Nitalima kwa juhudi ili nipate mavuno mengi', mkulima alisema

________________________________________

27. <u>**Kanusha sentensi**</u>
Mbwa alikunywa maziwa mengi

________________________________________

28. Neno jikalamu ni hali ya ukubwa wa neno kalamu
Tunga sentensi ukitumia hali ya udogo wa neno <u>kitanda</u>.

________________________________________

## VI. FASIHI

29. a) Eleza maana ya maneno yafuatayo (alama 2)
   i) Ploti ________________
   ii) Fasihi ________________

b) Visasili ni hadithi za kihistoria zinazosimulia kuhusu asili ya mambo fulani yanayohusu maisha ya binadamu. Taja mambo mawili yanayohusu visasili (alama 2)
   i) ________________
   ii) ________________

c) Eleza tofauti iliyopo kati ya hurafa na hekaya (alama 2)

________________________________________
________________________________________

d) Eleza umuhimu wa wahusika katika tamthilia. (alama 2)

________________________________________
________________________________________

e) Taja jina jingine la ploti katika fasihi (alama 1)

________________________________________

f) Andika sababu moja ya kuimba nyimbo za dini (Alama 1)

________________________________________

# TARGETER WINGS

## JUNIOR SCHOOL ASSESSMENT

# GREDI YA NANE - 2024

Wings 005

## SEHEMU B:

## KISWAHILI : INSHA

***MUDA: Dakika 40***

| | |
|---|---|
| **Jina** ______________________________ | |
| **Shule** ______________________________ | |
| **Nambari ya Usajili:** ________________ | **Tarehe** ________________ |

**SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI**

1. Kwenye nafasi zilizoachwa hapo juu **andika jina lako na jina la shule yako.**

2. Sasa fungua karatasi hii, soma kichwa cha insha kwa makini na uandike insha yako kwenye nafasi uliyoachiwa.

**Kijitabu hiki kina kurasa 4 zilizopigwa chapa.**

*© Hutungwa na kuchapishwa na Targeter Educational Publishers Ltd. Email:info@targeterpublishers.co.ke*

FUNGUA KURASA

*Andika insha ya maelezo kuhusu namna ya kuwahudumia watu wenye mahitaji maalumu katika familia.*